# HAKI ZA LUGHA:

# NAFASI KWENYE JUKWAA LA RIGHTSCON 2021!

Shirika la **Global Coalition for Language Rights** (GCLR) ni kikundi cha watu na mashirika yanayofanya kazi inayohusisha lugha na haki za binadamu. Lengo la kikundi hiki ni kuchangia katika juhudi za kimataifa za kuongeza uwezo wa kufikia maelezo/huduma muhimu na uwakilishaji sawa katika masuala yanayohusiana na teknolojia zaidi ya vizuizi vya lugha, pamoja na kubuni njia za kushughulikia changamoto za kijamii, kielimu, kiuchumi na kimazingira, ambazo zinahusisha wazungumzaji wa lugha zote, ikiwa ni pamoja na lugha za asili na lugha ambazo hazijawakilishwa ipasavyo.

Mojawapo ya matokeo dhahiri ya kwanza ya kazi ya Muungano wetu ilikuwa ni kushiriki katika **RightsCon 2021** —mkutano maarufu wa kimataifa kuhusu masuala ya haki za binadamu katika enzi ya kidijitali! Haya yalikuwa mafanikio yanayofurahisha mara dufu kwa sababu haki za lugha zilipewa nafasi katika mkutano huu wa kiwango cha juu.

Lengo kuu la kikao tulicholeta kwenye RightsCon, —*Kuambatisha Haki za Lugha kwenye Ulimwengu Dijitali*—lilikuwa ni kubaini jinsi kazi yetu ya pamoja inavyoathiriwa na masuala yanayohusiana na **utofauti wa lugha** na **vikwazo vya lugha** katika kupata maelezo na huduma muhimu. Malengo yetu hasa yalikuwa ni:

- Kutambua namna ambavyo haki za lugha na za dijitali zinahusiana;
- Kuwatia moyo washiriki kujumuisha haki za lugha wanapoendelea na kazi zao; na
- Kuanzisha mahusiano mapya na watetezi wa haki na mashirika ili tuweze kusaidiana katika kazi zetu.

Tuliwaalika washiriki wenye shauku ambao walichangia maarifa na kushiriki maoni yao katika muktadha wa **vikao sita vidogo vyenye mada mbalimbali**. Unaweza kupata hapa chini mambo muhimu tuliyojifunza katika kila kikao chenye mada.

## *Mambo muhimu tuliyojifunza:*

**Teknolojia na Haki za Dijitali**

- Hata ikiwa teknolojia inapatikana kwa lugha asili, watu bado wanaweza kuitumia kwa Kiingereza au lugha ya pili kwa sababu mbalimbali: uzoefu wa kutumia teknolojia kwa Kiingereza au kwa lugha ya pili kutokana na hitaji la msingi (kutojanibishwa); lugha isiyotumika katika eneo mahususi ikiwa ndiyo lugha chaguo-msingi ya mfumo kwenye kifaa; au tafsiri duni au uzoefu wa mtumiaji na muundo katika lugha inayotumika katika eneo mahususi.
- Ujanibishaji si rahisi kama kutafsiri. Ujanibishaji wa programu hasa unahitaji matayarisho ya kiufundi na kuweka miundo mbinu na ni lazima uzingatie miktadha ya maeneo kwa kuzingatia lugha, muundo na hata utendakazi wa msingi wa teknolojia hio.
- Kujenga imani ya watumiaji wateknolojia ni jambo muhimu. Zana iliyojanibishwa kwa njia inayofaa inajenga imani, na tafsiri isiyokamili au isiyo sahihi na muundo duni unaweza kusababisha usumbufu na hali ya kushuku. Imani ni muhimu sana hasa kwa teknolojia zinazoshughulikia usalama wa dijitali au wa kimwili, huduma za afya na data ya kibinafsi.

**Ufikiaji wa Maelezo na Elimu**

- Kuna ukosefu mkubwa wa ufahamu wa kiwango cha tatizo na athari zinazoambatana nayo.
- Ni muhimu kufanya uhamasishaji katika jamii zetu na katika kazi zetu.
- Ni muhimu kuhakikisha kuwa mashirika na jamii yanajitahidi kuwezesha watu kufikia maudhui ya elimu katika lugha zao za asili.

**Ufikiaji wa Huduma za Afya na Ushughulikiaji wa Hali ya Hatari**

- Lugha ni muhimu sana wakati wa kuzungumza na wafadhili na umma.

- Maelezo muhimu ya afya yanapaswa kutafsiriwa mapema, kwa mfano, Toronto ina maelezo mazuri sana ya kabla ya kuambukizwa COVID lakini maelezo kuhusu chanjo hayapatikani.
- Inaweza kuwa vigumu kutafsiri dhana kutokana na kazi yako mwenyewe kwa wafadhili ambao wanaweza kufadhili kazi hii kwa wafanyakazi wa huduma za afya au kwa umma.

**Mwongo wa Kimataifa wa Lugha za Asili**

- Ni kitu gani kinachotangulia? Kutumia mfumo dijitali ili kuifanya lugha "itambulike", au kukuza matumizi halisi ya lugha hiyo kwenye mtandao kutoka kwenye jamii?
- Ni muhimu kuzuia mitazamo ya kikoloni au inayotenga ambayo inaweza kusababisha "hali" hii au kufanya utafiti ili kupata maarifa haya bila kunufaisha jamii zenyewe.

**Haki, Uhamasishaji kuhusu Mazingira na Kushirikisha Raia**

- Toa tafsiri karibu na jamii, zenye uamuzi wa haraka kulingana na udharura wa miundo wima na kazi halisi;
- Zingatia miundo mbinu mingi ya kijamii ambayo inaweza kuwa tofauti kabisa na inayotokana na vipengele tofauti (kushiriki maelezo kwa njia ya kuzungumza ikilinganishwa na kuandika);
- Gundua njia bora zaidi za kushiriki maarifa na jamii za asili ili kuhakikisha kuwa wanaweza kuyafikia na kuchukua hatua/kujihusisa ipasavyo baada ya kupata maelezo kamili.

**Haki za kazi na Fursa za Kiuchumi**

- Katika eneo la Marekani Kusini, kuna viwango viwili vya vikwazo vya lugha: Watu wa asili wasiozungumza Kihispania (na katika baadhi ya nchi, Kireno na Kifaransa), watakumbana na changamoto ya kupata nafasi za kazi na kufikia uchumi rasmi. Pia, utandawazi umeweka kuwa kuzungumza Kiingereza si tu jambo la faida, lakini pia ni masharti ya kujiendeleza kikazi.
- Siku hizi, watu wengi wana ufahamu kuhusu vikwazo vya lugha vinavyopatikana kazini mwao, hata kama hawana uhakika kuhusu suluhisho. Kutambua mahitaji ya kufikia huduma za lugha ni hatua kubwa, lakini suluhisho zilizotolewa bado zinazingatia zaidi lugha zinazozungumzwa na wengi (Kifaransa, Kiingereza, Kihispania ni mifano iliyotolewa).
- Kuna mapendeleo fiche kwa kiwango kikubwa katika uendelezaji wa teknolojia na lugha ni mojawapo ya njia ambayo mapendeleo haya yanajitokeza. Kufanywa kiotomatiki kwa kazi zinazohusiana na lugha kunaweza kusababisha kupatikana kwa maelezo yasiyo sahihi, utofautishaji wa jinsia, n.k. Teknolojia imetambua mapendeleo haya; sasa ni wakati wa kuondoa mapendeleo haya yaliyokita mizizi katika zana zetu.

Unaweza pia kupata baadhi ya vyanzo vilivyotumika kutayarisha kikao hiki, katika hati yetu ya [Nyenzo zinazohusiana](#).

Tungependa kuwashukuru tena, washiriki wote kwa kuungana nasi na kuchangia kwenye mazungumzo yetu. Ilikuwa ni fahari na heshima kubwa kwetu kukutana nao na kujifunza mengi kutoka kwenu nyote.

# *Chukua Hatua!*

Ungependa kutoa **mchango kwa juhudi za Muungano wetu** kwa kufanya muhtasari huu ufikiwe kadri iwezekanavyo kupitia ujuzi wako wa kutafsiri? Tafadhali wasiliana nasi na utufahamishe kuhusu jinsi ambavyo ungependa kutoa mchango wako. Tutafurahi kupata maoni.

Usisite kuwasiliana nasi iwapo unafikiri kuwa kuna njia yoyote ambayo tunaweza kusaidiana.

Muhimu zaidi, unaweza kusaidia kwa kujitahidi kuendeleza ujumuishwaji wa lugha katika kazi yako. Unaweza kuwasiliana nasi wakati wowote katika **global.language.advocacy@gmail.com** ikiwa ungependa kujadili njia ambazo unaweza kufanya hivyo!

Pia, usisahau kutufuatilia kwenye **Twitter** katika @**GlobLangRights** ili kuongeza habari zinazohusiana na lugha kwenye mipasho yako uendelee kupata habari kuhusu mipango ya **Global Coalition for Language Rights!**